Muhtasari wa Mambo Muhimu

Jukumu la Tume ya Kuchunguza Ghasia za Baada ya Uchaguzi (CIPEV) lilikuwa kuchunguza sababu na mazingira ya utokeaji wa ghasia, jinsi vikosi vya usalama wa taifa vilivyozishughulikia na kutoa mapendekezo kuhusiana nayo na mengine.

Ripoti hii ina sehemu 5. Sehemu ya I ni utangulizi unaojadili muktadha wa kihistoria wa ghasia; sehemu ya II ni maelezo ya kina kuhusu ghasia mkoa baada ya mkoa; sehemu ya III inaangazia maswala manne yanayohusiana: dhuluma ya kimpaenzi, wakimbizi wa ndani kwa ndani, vyombo vya habari na hali na athari ya ghasia zenyewe. Sehemu ya IV inaangazia ulegevu wa vikosi vya usalama wa taifa na kutoadhibiwa kwa uvunjaji sheria na sehemu ya inajumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwa lengo la kuzuia utokeaji tena wa ghasia kwa kiwango kikubwa; uchunguzi wa washukiwa na jinsi ya kuikabili tabia ya kuvunja sheria bila hofu ya kutoadhibiwa ambayo imekuwa msingi wa ghasia na makosa mengine ya jinai nchini.

La kusikitisha ni kuwa, ghasia zimekuwa sehemu ya shughuli za uchaguzi nchini Kenya tangu kufufuliwa kwa siasa za vyama vingi mwaka wa 1991. Hata hivyo, ghasia zilizoitikisa Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 hazikutarajiwa. Kwa kiwango kikubwa zilikuwa mbaya na zenye uharibifu zaidi kuwahi kushuhudiwa nchini Kenya. Pia, tofauti na misururu mingine ya ghasia zinazohusiana na uchaguzi kuwahi kutokea, nyingi zilifuata badala ya kutangulia uchaguzi. Ghasia za baada ya uchaguzi 2007 – 2008 pia zilisambaa kuliko ilivyokuwa awali. Ziliathiri mikoa yote isipokuwa miwili na zilihisika kote kote mijini na mashambani mwa nchi. Awali, ghasia katika kipindi cha uchaguzi zilikolea katika wilaya chache haswa mikoa ya Bonde la Ufa, magharibi na Pwani.

Kuhusu tabia ya vikosi vya usalama wa kitaifa, vilishindwa kitaasisi kukadiria, kujiandaa na kukabili ghasia. Mara kwa mara, watu binafsi katika vikosi hivyo walishiriki matendo ya ghasia na ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu.

Kwa njia nyingine, ghasia za baada ya uchaguzi zilifanana na mizozo ya kikabila ya miaka ya 1990 na ilikuwa sehemu ya mkondo wa kuendeleza ghasia nchini Kenya kwa miaka mingi. Ukweli kwamba makundi haramu mengi ambayo yalichipuka katika mizozo hiyo ya kikabila, hayakuvunjiliwa mbali, kulipelekea urahisi wa kufufuliwa kwao na viongozi wa kisiasa na wafanyibiashara kwa minajili ya ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Pili, ubinafsishaji wa mamlaka ya urais unaendelea kuwa **kigezo** kikuu katika kurahisisha ghasia zinazohusiana na uchaguzi

Imani iliyoenea kwamba urais huleta manufaa kwa kabila la Rais hufanya jamii kutaka kutumia ghasia kupata na kuhifadhi mamlaka. Kukosekana kwa usawa na kutengwa kiuchumi kunafanywa mara nyingi kwa misingi ya maeneo ya kikabila kulichangia pakubwa katika ghasia za baada ya uchaguzi katika maeneo kama vile mitaa ya mabanda ya Nairobi.

Moja kati ya matokeo muhimu ya uchunguzi wa tume, ni kuwa ghasia za baada ya uchaguzi hazikupagwa katika maeneo fulani ingawa zilikuwa matokeo ya kupanga na kuratibiwa katika maeneo mengine, mara nyingi zikihusisha viongozi wa kisiasa na wafanyibiashara. Maeneo kadhaa yalishuhudia jumla ya aina mbili za ghasia, ambapo kilichoanza kama tetezi dhidi ya tuhuma za wizi wa kura baadaye zilibadilika na kuwa mashambulizi yaliyopangwa na kuratibiwa dhidi ya watu kutoka makundi ya kikabila yaliyohusiana na Rais au chama cha PNU. Hili lilifanyika kulikotarajiwa kwamba kungetokea ghasia kutokana na matokeo yoyote ya uchaguzi.

Ripoti inahitimisha kwamba ghasia za baada ya uchaguzi hazikuwa tu mgongano wa wananchi kwa wananchi. Huu ulikuwa uvamizi uliopangwa dhidi ya Wakenya kwa misingi ya makabila yao na walikoegemea kisiasa.

Wavamizi walijipanga katika makundi ya kikabila, waliratibu mbinu na kusafiri miendo mirefu kuchoma nyumba, kujeruhi, kuua na kudhulumu kimapenzi wakazi kwa sababu walengwa walikuwa wa kabila na mrengo fulani wa kisiasa. Kuhusishwa na watu ama jamii Fulani kulisababisha uvamizi mbaya wa kulipiza kisasi, huku wahasiriwa wakitambuliwa sio kwa walilolifanya bali kwa kuhusishwa kikabila na washukiwa wengine. Huu uhuru kwa wote uliwezekana kutokana na kukosekana kwa sheria kulichipuka kutokana na kukosekana na kushindwa kwa taasisi za kitaifa na vikosi vya usalama.

Kwa jumla, askari walizidiwa na idadi kubwa ya wavamizi na kufaulu kwa mipango yao ya mashambulizi. Hata hivyo, katika maeneo mengi ya nchi yaliyoathiriwa na ghasia kushindwa kwa upande wa polisi wa Kenya na utawala wa kimikoa kutekeleza habari za kiujasusi na dalili nyingine za kuonya za mapema kulichangia kuongezeka kwa ghasia. Ghasia za baada ya uchaguzi ni suala la kukosa kujiandaa, na ushirikiano mbaya miongoni mwa vikosi mbalimbali vya usalama wa kitaifa. Japo huduma ya kijasusi ya kitaifa kuhusu usalama ilionekana kuwa na taarifa ya kutekelezwa kuhusu uwezekano wa ghasia katika maeneo mengi ya nchi, haikuwa wazi endapo na kupitia kwa nani taarifa kama hiyo ilipashwa kwa vikosi vya huduma vya usalama. Uwezo wa polisi wa Kenya na polisi wa utawala uliathiriwa vibaya kutokana na kukosekana kwa utaratibu wa wazi wa sera za utendaji na athari kubwa ya kisiasa kuhusu sera zao muhimu.

Ripoti inapendekeza mbinu mwafaka za kuimarisha utendakazi na uwajibikaji wa vikosi vya usalama na kitaifa, na ushirikiano kati ya mifumo ya usalama wa kitaifa pamoja na kuimarisha mipango ya pamoja ya maandalizi ya utendaji, kujenga mifumo kamili ya udurusu ya utendakazi, kuunganisha vikosi hivyo viwili vya polisi, na kuzindua mamlaka huru ya malalamishi ya polisi.

Ili kimaliza tabia ya kutoadhibiwa kwa uvunjaji sheria ambako ndiko msingi wa ghasia za baada ya uchaguzi, ripoti inapendekeza kuundwa kwa mahakama maalum yenye jukumu la kushtaki makosa ya jinai yaliyotendwa kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi. Mahakama hiyo maalum itashirikisha wataalam wa kimataifa katika jopo kuu la uchunguzi na mashtaka mahakamani.